

CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

(CKRC)

Verbatim Report Of

**DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL, SABATIA
CONSTITUENCY, HELD AT VOKOLI GIRLS SECONDARY SCHOOL**

ON

9TH OCTOBER 2002

By Lilian Bango
Final Copy.

**DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL, SABATIA CONSTITUENCY, HELD AT VOKOLI
GIRLS SECONDARY SCHOOL ON
9TH OCTOBER 2002**

Present.

1. Com. Kavetsa Adagala

Secretariat Staff in Attendance

1. Vincent Wakato - Asst. Programme Officer
2. Patricia Mwangi - Verbatim Recorder
3. Agnes Ayuma - District Co-ordinator

3 C's:

1. Mr. Benard Chahilu - Chairman
2. Ms. Margaret Sabwa - Secretary
3. Jamen Andagalu - Member
4. Mrs. Mesceline Mirembe - Member
5. Mr. Wilson Saratia - Member
6. Mrs. Vukaya Kibira - Member
7. Mr. Joseph Vololi - Member
8. Mr. Ionui Isaiah - D.O.
9. His Worship Mayor J. Kivihya.

Meeting was called order 10.10 a.m.

Benard Chahilu: Commissioner Kavetsa, bwana D.O. na wageni ambao mmehudhuria mkutano huu, hamjambo.

Audience: Hatujambo.

Vincent Wakato: Nafikiri tumechelewa kidogo kwa hivyo tutaanza mkutano na maombi, nafikiri Mzee mmoja atatuombea

shule ambaye eh, kuja kuja mbele.

Prayer. Mzee Omwenyere: Tusimame tuombe. Asante Mwenyezi Mungu, tunakuomba wakati wa leo saa hizi siku ya Juma tano tariki wa tisa tushajua tunataka kutengeneza Katiba yetu ya Kenya iwe katika mkono wako la chini kabisa na umtajiri ambayo ulimpa Solomoni mtumishi wa kuadhamani na wote wataanzia nawaombea baraka ya Mungu ikae pamoja na hao na huu mkutano ijae kanisa hili, Mungu barikia kila mtu akiwa kwa njia akifika awe na amani na D.O wetu hapa, tunamuomba tena utakuwa pamoja naye na. Wote ambao Wakenya wote nawaombea baraka ya Mungu utawabariki nikiomba hii katika jina la Yesu Mkombozi mwema. Amen.

Benard Chahilu: Asante sana Mzee kwa maombi. Kwa niaba ya kamati ya Sabatia ya kutayarisha mambo ya Katiba, ninafuraha kukaribisheni nyote kwa kipindi hiki karibu cha mwisho kabisa katika harakati za kuunda Katiba yetu mpya. Hapo nyuma tulikutana hapa na tukatoa maoni yetu, na nina furaha ya kusema kwamba wale ambao mmesoma magazeti mmeona Katiba mpya imetoka. Hiyo Katiba mpya inaonyesha yale maneno ambao ninyi wenyewe mlitoa. Kwa hivyo wakati wa leo tutasikia Commissioner Kavetsa akitueleza ni namna gani walitayarisha hii na kutafsiri mambo fulani katika Katiba hii. Kwa hivyo leo ni kusikiliza na kutoa maoni na kusikia matafsiri za section tofauti tofauti katika Katiba mpya muwe huru kuuliza maswali, muwe huru kutoa maoni kwa sababu hii ni wajibu wenu kama wananchi wa Kenya. Kwa hayo machache nafikiri nitarudisha kazi hii kwa Commissioner Kavetsa atuongoze kwa sababu yeye ndio mwenyewe na sisi tutasikia yale yatatoka kwake. Asante sana Commissioner.

Com. Adagala: *(In Kiluhya)*

Audience: *(In Kiluhya)*

Com. Adagala: *(In Kilihya)* Vincent ni Programme Officer *(In Kilihya)* ni Patricia Mwangi *(In Kiluhya)* Verbatim Reporter. *(In Kiluhya)*.

Speaker: The tape should not be so far away.

Com. Adagala: *(In Kiluhya)* This is the other one, it's not bad, it's okay, I want to give them a background of the report. *(In Kiluhya)* give me one of your copies for Sabatia, do you have Sabatia? *(In Kiluhya)*. Chair, where is chair with your committee? Please come forward with your committee, I want to hand this over to you. I want to give you the report as you talked, as your people talked. Yeah, come the committee, take that camera where is the camera(?). *(In Kiluhya)* . Do you have a camera District Coordinator? Who has a camera? Ah, *(In Kiluhya)* report number one, one one.

Speaker: One.

Com. Adagala: Yeah, report number 165 Yeah, Sabatia. (*In Kiluhya*) your copy madam, yeah (*In Kiluhya*) District Coordinator (*In Kiluhya*) you want us to give them two or you want to remain with one? Yeah, (*In Kiluhya*) na do you have a place, a documentation center somewhere?

Vincent Wakato: Yeah.

Com. Adagala: (*In Kiluhya*). Tume yetu haina vikwazo baina sisi na nyinyi, hakuna kitu hakuna mtu kati ya sisi hati middle man au mtu ambaye tutapitia ni wananchi na nyinyi, peke yake. Kenya hii kuna vitu viwili muhimu pekee yake, na nataka msikie. Kuna vitu viwili muhimu peke yake, wananchi na Katiba. The people and the Constitution, wananchi wanatengeneza Constitution kuwalinda na wananchi ndio wanalinda constitution, muelewe. Hakuna mtu mwingine atalinda Constitution, ni wananchi. Kila mwananchi lazima alinde constitution kama ulitioa maneno iko hapa utayalinda na pia kama unaona kuna jambo hapa bado linakuinga maisha yako au kukusaidia kwa maisha yako, utakinga Katiba. Hakuna sio hii Katiba nani atafanya hii, hakuna nani, eh, (*In Kiluhya*) ni hapa tu, wananchi na Katiba, vitu viwili peke yake, okay. Tutazungumza hiyo baadaye.

Nataka kumpa chair hapa ah, come and hold the mic for me yeah, natakaI want to the photograph, did you get the(?) okay hii kamati imekuwa active (*In Kiluhya*). Hii kamati imefanya kazi, kamati ya Sabatia eh, you have to take like this. Take the date then you will take the picture. Hi kamati imefanya kazi, kazi yao tumeiona hata District Coordinator anatufanyia na pia watu wakwanza kupongeza commission tuliporudi Mombasa, District Coordinator alipiga simu akatuambia mmepokea ile Katiba ilikuwa kwa gazeti, ile report ilikuwa kwa gazeti kwa moyo wote na mmeona ni repiti nzuri iko na vitu vile mmesema na tulikuwa tumekaa kwa plenary, tulikuwa kama tumekufa moyo kidogo lakini kila mtu alifurahi hata Professor Ghai nilimwambia oh, District Coordinator has rang and said that the people are very happy with the report. Then akasema oh really, really this is very good. Akacheka kwa sababu hatukuwa tunacheka kwa hiyo plenary tulikuwa na kazi nyingi, mahakama wanatusumbua, wanasema tutaenda jela, tutasema tutaenda okay. Haya ndio hii Katiba, mchango wenu wa Katiba ndio huo na (*Clapping of hands from the audience*) na hata tumefurahi tumefurahi sana. Haya asante, au una kitu kingine.

Mr. Chahihu: Mimi kwa niaba ya kamati, ninataka pia kupongeza Commission kwa kututambua na kutupatia nakiri ya Katiba mpya na nataka kuandika nyote ambao mko hapa na wengine mje mbane documentation centre tutaweka nakala hii kule muweze kusoma yale maneno ambayo mnaenda na kufanya photocopy na mpeleke nyumbani mtumie. Asante sana, na hii nyingine photocopy. Kwa hivyo Commissioner Kavetsa tunashukuru sana kwa kutupatia nakala ya Katiba mpya ya Kenya. Asante sana. Commissioner kabla hatujaendelea ningetaka bwana D.O naye atukaribishe kwake. Bwana D.O.

Mr. Tonui (D.O): Okay, asante, yangu sina mengi nikukaribisha wageni wetu ambao wamekuja tuangalie draft constitution ambao mlipiana maoni yenu. Nafikiri mtaongea bila wasi wasi, wengine wenu wamesoma wengine bado, lakini nyote tuko nazo hapa so karibuni hapa Sabatia. Sisi hatuna shida mimi binafsi sijaona kitu kibaya kwa hiyo Katiba na bado nisoma area

zingine. So asanteni, karibuni.

Com. Adagala: Haya asante sana tumeshukuru. Chief ako wapi? Chief wa Odanga, ametoka? Okay. Njoo useme tuweke kwa..

Area Chief: Asante sana bwana D.O., Commissioner Kavetsa na wengine. Hamjambo. hamjambo tena.

Audience: Hatujambo.

Area Chief: Hamjambo tena.

Audience: Hatujambo.

Area Chief: Mimi nawakaribisha hapa kwa location hii, yote ambayo mtanena itakuwa ya manufaa ya Kenya nzima. Kwa sababu ningependa muwe free, mtoe maoni yenu ambayo itasaidia wote Wanakenya. Asanteni sana.

Com. Adagala: Headmistress hako, hajaingia? Headmistress ameingia wasichana? Okay akija mnijulize. Okay area officer ako wapi? Education Officer, A.E.O, ako wapi? Nilimtuma lakini nilitaka aende na hii gari. Sasa ako wapi? Ako Sabatia kuna mtu anaweza kwenda na Dereva amtafute huko Sabatia? Nilimtuma apelike Katiba kwa secondary schools. Who can go with him, D.O. who can go with him the driver to Sabatia? Who knows him? He is here? Call him please. Okay. Are you going? Just know, okay call my driver for me. Two copies for every high school, okay sasa tunaendelea na tutataka tuanze rasmi.

Hiki ni kikao cha Tume ya Kurekebisha Katiba hii ni mara yetu ya pili Vokoli, lakini ni mara tatu au inne hapa Sabatia. Sasa tumekuja hapa, tulikuwa hapa tukachukua (*In Kiluhya*). Wasichana mtakuwa kimya, wasichana okay, kazi yetu ni ngumu sana msifanye ngumu zaidi okay. Ni kazi ngumu sana ninaweza kuwaambia kwa sababu nimefanya kazi nyingi duniani hii, hakuna kazi ingine ngumu kama hii. Sasa mkikimia tukizungumza itakuwa sawa au to mtu yeyote akizungumza itakuwa bora.

Tulikuwa hapa tukafanya Civic Education, nafikiri Commissioner Kangu na Commissioner Baraza walikuwa huku wakati huo, pia tulikuwa kwa Province tukafanya launching mbeleni na tukafanya pia district civic Education na tukachukua pia maoni ya NGO's na CBO's mbeleni. Halafu tukaja tukafanya civic education nafikiri venue ilikuwa chamakanga na district coordinator, Chavakanga na Jivanzi na Kidondo. Yeah hapa hatukuweka na lakini tukipokuja kufanya hearings, nilisema watu wa Western ni watu wengi kuna population nyingi tufanye three venues kwa kila constituency. Na mahali pengine kulifanya three venues kwa kila constituency are the dry areas or the Pastoralists areas kwa sababu watu wako mbali mbali na pia wana maisha yao ya kutembea tembea na mifugo yao hiyo pia ikafanya hivyo, lakini hapa Western tulikuwa na three venues almost everywhere. I

think Vihiga constituency we had two but the other constituency here in Vihiga district we had three each, okay. Sasa tukaongeza Vokoli, tukasema Vokoli unaweza tu sign na watu wanakuja na kweli mlikuja kwa wingi.

Siku hiyo, siku ya Civic Education ilikuwa yetu ya kuzungumza na siku ya hearing ilikuwa yenu sivyo, kwa sababu inafaa mkubali ni nyinyi ndio mlikuwa mnazungumza, tuliandika sisi Commissioners tulikuwa na Professor Salim na Pheobe Asiyoy tukaandika halafu tukaweka kwa tapes, hizo tapes zote huyu ndio mkubwa wa hiyo section ya Verbatim Reporting, hizo tapes zote ziko kwa Library. Where are they stored?

Patricia Mwangi: In the Library.

Com. Adagala: In the documentation centre of the Commission, ukitaka kusikia sauti yako iko huko. Halafu huyu na department yake, huyu Patricia Mwangi na department yake wanaandika kila neno na waliandika kila neno, ukitaka kuona original utaiona, iko pia kwa report.

Sasa tumerudi, tulienda vile tulitoka hapa Western ndio ilikuwa ya mwisho na mnajua huko Western ukienda alphabetically Vihiga ndio ya mwisho, sivyo. Sasa hapa ndio ilikuwa ya mwisho tukaenda na tukachukua maneno mlichanga yote, hayo maoni, pendekezo na tukaweka pamoja tukaenda Mombasa. Tuliweka kwa computer hiyo mambo yote na ukiwa ulitoa maneno kuhusu elimu iliandikwa hapo, iliwekwa watu wa elimu wametoa, watu wametoa watu kadha na hakuna mahali pengine elimu ndio ilichangiwa kuliko ingine yeyote.

Hayo mambo mnasikia ya mahakama ya Judges, mlizungumzia hapa, sivyo? Yeah, Kenya nzima kwa kuandika hiyo maoni ni ukurasa elfu moja mia nane, ukurasa hivi yaani iko hivi. Hiyo ni kama 2000 ni kusema ni how many reams? 8 reams, hiyo 8 reams ya paper ndio maoni kuhusu mahakama. Na mnaona wanataka tusizungumzie, hiyo ndio walikuwa wanasema, Wakenya wasizungumzie hayo mambo. Na hiyo ni kupiga marufuku, unajua sasa Wakenya wote ni kama watu ambao wanahatia kwa sababu tunazungumzia na sisi wakasema tuende jela tukasema tutaenda.

Professor Ghai akasema vile nilizalia Ruiru, hata nikienda Kamiti Maximum itakuwa karibu na nyumbani. Haya, Hoteli ingine huko Five Star, Hotel Intercontinental ikasema mkienda tutawafanyia outside catering yaani watatuletea chakula. Sasa tulikuwa tu na moyo wa kuendelea na kweli tulikata mambo ya Mahakama kwa sababu Mahakama haina ruhusa kusimamisha mambo ya Katiba. Hiyo si jukumu yao, okay wao wako ndani ya Katiba sasa dhidi watasimamisha Katiba yote. Haiwezekani hao ni sehemu ndogo ya Katiba. Lakini pengine niwaeleza kwa sababu siku ya leo ilikuwa Wakili wote watasusia kwenda kwa Mahakama ndio tumevaa hii, hii imetoka kwao, kwa Mawakili wanasema ukivaa hii unakubali na mambo ya Katiba. Kama hukubali na mambo ya Katiba usivae, kwa sababu Katiba ni kitu (*In Kiluhya*) is something to be believed in, so if you don't believe don't wear it, na hatuwezi kukuforce, hata nitatangaza tena ili wale ambao wamevaa pale bila kujua watoe, okay. Na wale wamevaa mjue mnavaa uweke hii kitu vizuri sana, ukaweke uwe unavaa siku nyingi. Okay, haya so ndio hiyo

tutazungumzia ya Mahakama na tumweleze ni nini inaendelea hapo lakini hasa hawkutaka mtu yeyote azungumze mambo yao na nyinyi ndio mlituambia sivyo?

Audience: Yeah.

Com. Adagala: Sasa tulitoa wapi hayo mambo?

Speaker: Kwetu sisi.

Com. Adagala: Yeah, so mtu wa Vihiga akisema kama wanataka kutupeleka Kortini watupeleke sisi wananchi kortini, kwa sababu sisi ndio tulitoa maoni. Yeah, so anyway waliambiwa na kamati ya Parliament ya Bunge ambayo inatusimamia ambayo chairman ni Hon. Raila Odinga wakaambiwa wakitaka kushtaki, wasishtaki mtoto-Commission, washtaki mzazi Parliament, Bunge watoshane kwa sababu wanatoshana. Bunge mahakama na urais hiyo yote inatoshana, wao ndio brothers, sasa sisi tuko sawa kwa sababu yote inaenda kwa clerk of National Assembly. So, hiyo ni hivyo lakini kitu tu hawakutaka wawekwe kwa category moja na wananchi. Hawakutaka wakaguliwe ulikuwa unafanya kazi ipi? Kazi yako pengine una.. kustaafu ni miaka 74 lakini tunataka iwe 65 hiyo kitu.

Hatu huyo D.O. amekubaliwa kukaguliwa eh, na lazima kwa sababu ninyi ndio mlikuwa mnakagua na sisi tuliweka tulichanga pamoja halafu tukaenda Mombasa ilikuwa kwa hiyo story. Tukaenda Mombasa, Mombasa ilikuwa kazi ngumu sana, tulienda kukaa kwa Hoteli ya Peter Rudava alikuwa huko Manager. Si mlijua alikuwa Dish Lodge? Yeah, na tulifanya huko kazi hata wakashangaa hatujaona watu ambao wanafanya kazi usiku na mchana kama hii commission.

Halafu pia tuliko.. kwanza Bahari ilikuwa kama hapa barabara sikukanyaga hata siku moja mimi. Sikukanyaga hata siku moja kwa sababu nilienda nikichelewa kwa sababu tulikuwa tunamaliza mambo ya Mzee hapa na wengine wakaenda Mombasa sasa nilipofika kule nilikuwa na kazi nyingi sana ya kufanya, ya ku-catch up. So hata watu hawaku.. tulifanya usiku na mchana na pia tulikuwa hapo na majadiliano ya ajabu. Mnajua Commission iko kidogo kama coalition, ndio hiyo ya mseto eh ya National Unity, sasa hapo ndio mambo yote iko, arguments kila kitu kiko hapo. So tulikuwa tunajaribu na kwa Kiluhya mnasema (*In Kiluhya*) consensus (*In Kiluhya*) yes, hiyo ndio system Constitutional Review Commission na iko kwa act, iko kwa sheria yetu. Kila kitu tujaribu as far as possible by consensus, voting hata tukivote issue moja halafu watu wakaenda inje mseme kwa nini tumevote hiyo na hizi zingine hatukuvote tena tukaenda the whole afternoon tukasikizana halafu ikaendelea.

Inafaa hiyo iweko kwa mila ya Waluhya, Wamaragoli iko na inafaa kila mahali na maisha itakuwa hivyo, democracia iko hivyo ni kuzungumza mnazungumza mpaka mnasililizana sio unazungumza huyo anazungumza na unachukua fimbo eh, na mwingine anachukua shoka eh (*In Kiluhya*). So hiyo ndio njia, hiyo ya consensus tulimaliza hapo tukaandika report eh, is there a copy of the report? I had put it away I don't think it is here. Do you have a report? No no the short version, short version. Hii report

ilikuwa kwa tarehe nini ya tarehe 27 magazeti, kama mtu alinunua. Wangapi walinunua hiyo gazette? (*In Kiluhya*) na tano (*In Kiluhya*). Okay, ndio hii you have a right to information, ours was not to take our report to anywhere our law told us, the act told us, you will release the report to the public, haikupitia mahali kwingine kwa sababu Bunge ilijua, ikienda Bunge kwanza au iende hapa kwanza au kule kwanza itakwama, akasema direct to wananchi. Na tulilete ikawa kwa magazeti na pia iko kwa District Coordinator nafikiri anaonekana kadha atawapea.

Halafu tukarudi Kencom House na hatukuwa tumemaliza pia tukafanya hapo tulikuwa tunatoka ofisini saa saba, saa tano, saa tisa ya usiku, saa kumi na unarudi saa mbili na unaanza kazi tena kwa sababu tunakuwa na vitu muhimu ambavyo vinaitwa transitional and consequential provisions. Daraja ya Katiba ya sasa na Katiba ambayo imependekezwa ilifaa tufanye hivyo ilikuwa vitu ngumu sana, sana sana na nitawambia tukiendelea ilikuwa aje.

Sasa hiyo hazi yetu temezoe, tumezoe hata tulikuwa tunatoka kazini saa tisa, ilikuwa kama hata (*In Kiluhya*) unaenda unajilazimisha kulala kwa sababu ubongo bado unafanya kazi. Unajilazimisha kulala halafu ni kama mtoto ako kwa mtihani eh, halafu unaamka unaamka inakupiga ubongo emeamka umavaa nguo umeenda eh, kwa sababu ukikosa utapata wengine wameendelea na kazi. Sasa ilikuwa hivyo, na tulifurahi kwa sababu ilikuwa kazi ya kutia moyo kwa sababu tulijua tunafanya kazi ya Kenya, ya Wanakenya na tulijua pia tunafanya kazi ya maana ya kutengeneza Kenya mpya. Nataka watu wajue hivyo Katiba mpya ni Kenya mpya, okay. New Constitution, New Kenya na tutaeleza kwa nini hata hiyo kwa jina Constitution wale mnajua lugha Constitution, constitute so hiyo tutazungumzia.

Sasa tuko hapa kuwaletea reporti yenu na pia kumpletea reporti ya Kenya nzima hii short version ingine iko, hii ni short version long version iko four volumes. Sasa hiyo ni kitu kama hivi lakini tukaona wananchi sasa hiyo ni kitu kikubwa kwa wao kusoma tukaandika hii na pia tumewaletea Katiba yangu iko hivi lakini ile mnapata kila mtu anayo. Hebu tuone watu wangapi wana Katiba hiyo ya Newspaper. Kuna wengine hawana?

Audience: Wengine hatungali hatujapata.

Com. Adagala: Eh.

Audience: Wengine hatungali hatujapata.

Com. Adagala: Kama hukupata, haukuregister, mume register?

Audience: Tumeregister.

Com. Adagala: Please eh, how come people didn't get? District Coordinator, Chairman, how come people didn't get?

Benard Chahihu:(Inaudible).

Com. Adagala: Okay, okay gari itarudi inavitu vingine, gari letu ni office sasa viko kwa office ya gari. Msifikirie hili gari ni langu, hii ni office, natembea na offices hawa na mimi na vitu vyote na hii yote ndani. Sasa sio gari langu binafsi, haya tutapata haya. Haya nafikiri nawambia kwa ufupi, lakini nataka kumwambia tu kitu kimoja mkizungumza, excuse me District Coordinator kama wanazungumza wacha. Enza Agnes wacha, wacha wacha. Agnes stop please. Nataka heshima ya kuzungumza na nataka heshima ya kila mtu kuzungumza lakini mkitaka ngu, mkianza ngu! ngu! ngu! inanitatiza (*In Kiluhya*) kwa nini unasema ngu! ngu! ngu! hamtaki? Eh.

Audience: Hakuna kungangania.

Com. Adagala: Hakuna kungangania kwa Katiba, hiyo ni tabia ya 20th century, tuko 21st century. There are objectives of the Review, nataka tufanye hiyo sasa ni kama tunarudia. Kwa objective zetu kuna sababu fulani tumefanya hii kazi. Ya kwanza wananchi maisha yao waliona maishani mwao haindelei vizuri na iliendelea ikazoroteka na hukujua kwa nini. Halafu wataalam, kwa sababu watu walikuwa wananungunika vitu fulani wanaambiwa hiyo ni mambo ya Katiba na mwishowe tukafika wataalam wakatuambia lazima tusililize mambo ya wananchi, maisha yao haendelei vizuri hata kutoka 1963 tumeendelea kuwa poorer, poorer and poorer sasa hata watoto percentage fulani hawaendi shule, watu hawana matibabu na imeendelea kuharibika, sasa hiyo ni sababu moja kwa sababu maisha yenu yenyewe hayakuwa inaendelea vizuri.

La pili, tangu sitini na tatu maisha imebadilika hata ni Historia miaka arobaini inafaa tuko kwa enzi mpya, tuko kwa maisha mapya, sasa ilionekana lazima tuangalie tena Kenya inaenda vipi, hiyo ni sababu ingine. Hata nyinyi wenyewe, wazee wanajua maisha imebadilika hata vijana wenyewe wameona kidogo wale wako kama 30 years wameona kuna tofauti so it is responding to the modern times, to the contemporary times. What is going on in our lives now and how did things change from 63 na hiyo ni Historia lazima kila mara hata tumeweka kwa Katiba kila mara lazima Katiba iwe inakaguliwa iwe inakaguliwa, watu walisema tutasema iwekwe iko kwa report.

Na pengine hata tulichelewa kwa sababu nchi zingine zilipata Katiba zilibadilisha. They just got independence and set to changing the Constitution kwa sababu hii Constitution tunayo ni ya makaburu ya sasa eh, hata inasema Kenya is a republic lakinin haisemi kitu chochote kuhusu watu wa Kenya. Ni kama sasa ni ramani tu, ni map bas. Haya ndio hiyo pia tukaona tuchange na vile ilitengenezewa London na hatukushiriki sana tulikata uhuru sasa tukaona pia hiyo ilikuwa mbali sana na mwananchi. Watu walienda kweli wa Bunge fulani walienda hata wengine bado wako hai nafikiri hata Mzee Otiende alienda mara moja hivi na tukaona wachu turudishie wananchi ndio tukaja na Civic Education, tukaja na hearings, wachange tutengeneze Katiba yetu. Mkiangalia kwa Katiba inaanza na we the people of Kenya. Hii ingine ilianza na Kenya is a sovereign republic, mnaona sasa tulikuwa na haja ya wananchi kutengeneza Katiba yao, hii ingine hawakutengeneza.

Sababu nyingine ni Katiba ya sasa nafikiri pengine 10% of Kenyans ndio wanajua na pengine ni Wakili, hata hiyo Katiba ukichukua ukianza kuisoma chapter mbili hivi ah, (*In Kiluhya*) what is this? Kwa sababu ina mambo magumu, lugha ngumu halafu hata hauwezi kufuata vizuri hata Professor Ghai mwenyewe amesema, hii Katiba ni ngumu sana hata hii ya leo, hata yeye mwenyewe saa zingine anashindwa kusoma, sasa Mtaalam wa Wataalam anashindwa, wewe mwananchi utaweza?

Audience:(Inaudible).

Com. Adagala: Utaweza?

Audience:(Inaudible).

Com. Adagala: Haya so ikaendelea ikawa lazima tutengeneze Katiba ambayo wananchi wanajua, kweli tungeita Wakili kumi na kuwaambia ketini hapo na wangeleta Katiba kwa miezi mitano hivi, lakini pia tungekuwa hapo hapo kwa sababu ingekuwa sisi hatujui na hatukushiriki. Sasa ndio tukasema wacha wananchi wenyewe wachange watu Wakenya wana akili na vile Mswahili anasema, kila mtu ana nywele zake sivyo eh kila mtu ana nywele zake. Sasa kila mtu ana akili sio watu fulani tu ndio wana akili peke yake. Ndio hiyo aspect ikatengenezwa na tukafika kuwaelimisha, kwa sababu watu hawajui Katiba ni nini. Ni kama kuwa Mkristo na usomi bibilia, na hausikii mambo ya bibilia, hakuna mtu anakuhubiria, wewe ni Mkristo kweli?

Audience: La.

Com. Adagala: Au sema uki Muislamu na Quoran hujui, wewe ni Muislamu kweli?

Audience: La.

Com. Adagala: Mmni hatulinganishi Katiba ya Mungu na hii yetu, lakini tu hauwezi kuishi na hujui nini inapanga maisha yako, sasa ndio tulifika kwa nyinyi tukafanya hivyo. Parliament ilitengeneza hiyo act, sisi hatuna hata hatua moja tunaweza kuchukua kwa Commission bila kufuata hiyo sheria, hakuna hatuwezi watu wanatuuliza oh, lakini Bunge ikivunjika sasa Katiba itakuwa nini? Tunawaambia hatuwezi kuvunja Bunge au teseme isivunjwe, hiyo ni mambo ya Katiba. Katiba ya sasa inasema President ndio anaweza kuvunja Katiba ya sasa ile iko.

Katiba mpya ni tofauti inasema bunge itakuwa na calendar yenyewe, ambayo itasimamia vile wataendelea. Sasa pia ndio tuliona tubadilishe tuje tusikilize na nyinyi tulifanya application sisi hii ni kazi tumeajiriwa Commission na kutoka huko watu 29 na tunafanya kazi. Sasa vile mnaona ni haja kubadilisha Katiba, ubayo wenyewe ni wananchi hawakujua Katiba yao, hata nikiuliza hapa nani ameona Katiba ya sasa hata wakati huu na nini, na macho hivi, kuona tu, ni watu wangapi? No put up your hand

kama umeiona na macho tu hata si kusoma, kuiona tu na macho.

Speaker:(Inaudible).

Com. Adagala: Sasa vile tunaendelea tunajaribu kuwaletea Katiba na tumewaletea hii ya Kiingereza, ya Kiswahili iko bado hawajamaliza tafsiri, itakuja itakuwa kwa magazeti pia hala tutatuma nakala zingine. Vile mko hapa every constituency itapata tu 200 copies kwa sasa okay, sasa ukipata si yako maisha ya mbeleni sio ya kuficha information, don't put it in your house, it is for other people to read also. Mtu akija mnasoma uweke vizuri lakini watu wasome. Sasa kwa Kijiji kama umetoka kwa Kijiji, make sure people read, vile ni ile tumeachia wasichana hapa wasome na mjadiliane hii si mambo ya kuficha wala hautapata kitu juu yake, ni ya kujua watu wote wajue ile maisha yetu indelee vizuri.

Ah, what is this? Okay mtanisamehe sijui ni kunisamehe au nilipasuliwa macho hata nilipokuwa hapa sikuwa naona hata mazishi ya Mzee sikua naona (*In Kiluhya*) ni kama miujiza yeah, sasa nafikiri najua Yesu alakuwa anafanyi nini alipotema mate na kutengeneza hapa, alikuwa anatengeneza lense ya kuweka ndani na kutengeneza hiyo konia ya kuweka ndani lakini hii ni Mungu kwa udongo alitumba sivyo?

Audience:(Inaudible).

Com. Adagala: Pia kwa udongo anaweza kuumba (*endolo*) sivyo? Yeah na mimi nimeshukuru sana hata nimeona Mungu amenibariki sana sana kwa hayo mambo.

Ah, na shukuru kanisa la Vokoli na hospitali yao, nimeshukuru sana (*In Kiluhya*) hata operation, yenyewe ilikuwa twenty minutes na wakaweka wakatoa asubuhi nikaona, ni kama mujiza kabisa. Haya sasa mko na nakala, mko na nakala ya Katiba, okay Headmistress we are in your queendom, we are in your place please come forward. We don't have any nakala here let me give here photocopy,(?) give me photocopy moja. We are very hapy to be here, we are very happy to be here for the second time na mlitukaribisha vizuri tufurahi, tukatoa maoni na tumetoa constituency report, pia tumekupa nakala kadhaa ya wasichana wako. Hii Katiba hasa ni ya vijana, wasichana na wavulana kwa sababu sisi tuko njiani, lakini tuwawachie Kenya nzuri, tuwawachie Kenya ambayo ina maana waishi bora kuliko sisi sivyo?

Audience: Ndio.

Com. Adagala: I think that is what it is, the world should be a better place eh, na kuna vitu vingine hapa watu wanasema is idealism na utopia and romantism na tuliwaambia eh, you must dream in life eh. Hata when you fall in love you want that love to go on isn't it?

Audience:(?).

Com. Adagala: But when you get married you want that marriage to be good, it may not be good but you dream, isn't it?

Audience:(?).

Com. Adagala: That it should be good, na hata hivyo kwa bibilia tumeambiwa thy kingdom come, isn't it?

Audience:(?).

Com. Adagala: Hiyo ndio pia tunataka maisha yawe mazuri, Mungu atubariki Kenya yetu iwe nzuri, okay. Haya hii ni nakala ya Library inaweza kufanyiwa photocopies na mtu yeyote na lakini weka kwa Library you don't have a photocopier there, yeah okay, yes yeah. You can make some photocopies someone comes, we want this to be a centre also. Someone people come and you give them, yeah if you have a few you know how much it will cost, so do that okay. Thank you very much God bless, God bless thank you so much.(?) karibisha.

Theresia Mbelase (Headmistress): Thank you Commissioner Adagala, D.O. Sabatia, Wazee na akina mama na wanafunzi hamjambo?

Audience: Hatujambo.

Theresia Mbelase (Headmistress): Hamjambo tena.

Audience: Hatujambo.

Theresia Mbelase (Headmistress): Mimi niko na furaha ya kuwakaribisheni hapa Vokoli school tumekuwa na bahati kwa sababu hii imekuwa centre ya mambo ya Katiba mpya na tumefaidika kwa sababu imekuwa rahisi kuja kukaa hapa kusikia maoni ya watu wengine tumefurahia, na tunaomba Mungu aendeleo kubariki hii kazi ili vile watakuwa wamemaliza, yatakuwa maneno yenye Mungu amebariki tusaidie Kenya hii tuwe na Kenya nzuri. Kwa hivyo mmekaribishwa sana. Asanteni.

Com. Adagala: Mungu akubariki na wasichana wako na shule yako. Ulisema jina lako kweli, yeah put your name on here for recording and for(?) say your name and your(?)

Theresia Mbelase (Headmistress): Kwa jina naitwa Bi. Mbelase, Principal Moi Girls Vokoli.

Com. Adagala: Thank you very much.

Speaker: Commissioner Adagala.

Com. Adagala: Mzee tafadhali, tafadhali Mzee.

Speaker:(Inaudible).

Com. Adagala: Keti keti yeah, mkifanya kelele nitaenda.

Speaker:(Inaudible).

Com. Adagala: Nitaenda tu, mkifanya kelele kingi, nitaenda, tutaenda niwaawache. District Coordinator chairman, are there nakalas there Margaret, Margaret not yet Yeah. (*In Kiluhya*). Those few of you who don't have you can share (*end of side A*).

Kwanza ile nimesema kuna mtu yeyote ana comment? Is there a comment or a question kwa yale yote nimesema? Hii ni wazi.

Speaker: Comment.

Com. Adagala: Comment come forward. Kuja forward, come forward hapa. Committee Members, who is your youth on your committee.

Speaker: Commissioner Adagala.

Com. Adagala: Tafadhali Mzee, poa. Who is your youth, who can do this for me, I want someone (*In Kiluhya*). Mzee rudi hapa please, nataka upoe tu hapa. Nani, I want someone on the committee who can be very quick.

Speaker:(?).

Com. Adagala: Where is he Jamii hey, (*In Kiluhya*) vile tunafanya si ki nini (*In Kiluhya*). Okay, we have only one microphone, so you will move back and forward.

Hezekiah Chesi: Jina langu naitwa Hezekiah Chesi mimi ni jua kali facilitator wa Constitution ya Kenya Review Commission. Nimekuwa hapa tumefunza sana hata wakina D.O. wetu hapa anajua, na complain yangu sijapata kufanya namna gani hiyo,

hakuna complain ni kupata Constitution hii mpya, hii kupata tu kitabu ya Constitution hii mpya. Hakuna maneno.

Com. Adagala: Chesi, Chesi nimesema Katiba zitarudi share with that person. Two wewe kama mkubwa wa jua kali ungenunua Standard au Nation na uwe nayo kwa ofisi yenu, ulinunua?

Laughter from the audience.

Com. Adagala: Haya okay. (*In Kiluhya*). Wacha tuvumilie na Kiswahili kwa sababu wanasema Kimaragoli ndio the nearest language to Kiswahili, mlijua hivyo? It the nearest Bantu language to Kiswahili, hamkujua? Haya okay, so mkiangalia kwa table of contents, table of contents. Yes, Peter come forward if you have a question you just come forward, you have to speak from the microphone.

Peter Ludava: I think I will avoid protocol to spread up. Nilikuwa nauliza, ni clarification kidogo tu. Hii nakala ambayo tuko nayo, ambayo ilitoka kwa gazeti na umesema iko tena nakala zingine kama volumes, sijui kama nne. Sasa kuna tofauti gani ya hii nakala ambayo tuko nayo ya gazeti na zile nne ambazo unasema ziko. Asante.

Com. Adagala: What is your name?

Peter Ludava: Jina langu ni Peter Ludava, I am a businessman.

Com. Adagala: Ah, okay wacha nieleze. Kuna nakala, excuse me I am answering a question to Ludava. Kuna nakala nne hiyo ndio long report, it is in four chapters, ah four parts. Hiyo kubwa tulifanya short version ndio hii, tuseme popular version, tulifupisha tukaweka hapa, okay. Kwa hivyo sijui mipango sana kuhusu hiyo lakini nafikiri itakuwa kwa Libraries na documentation centres na iko na details nyingi lakini hii ni summary, tuseme hii ni executive summary hii yeah. Ndio hiyo tofauti, okay those are the things we have put out in the public, report hii hii iko in the public na hiyo volume nne itakuwa pia, hiyo itachukua muda kupublish.

Halafu tumeweka hiyo nakala mnayo ya Kiingereza ya constitution okay, ya Kiswahili wako karibu kumaliza tafsiri na itawekwa tena kwa magazeti na kwa documentation centres in every district okay and it will be distributed, mnaelewa? Okay.

For this constituency, we have 200 copies na probably people who will come here will get it and then it will be finished, so you should not keep it to yourself. You must keep, you must share it, si yako personal, you must share it okay. Later own tutajaribu na baadaye tutachapisha constitution ili kila mwananchi awe nayo, where is that kapocket please? Na pia baadaye hata constitution ya zamani public law institute ilikuwa imeakuwa imetengeneza nakala hizi, hii na hii ya Kiswahili na Kiingereza inaitwa pocket constitution hii, pocket constitution hii inaweza constitution kufupishwa iwe hivi, ili unaweka hapo au kwa pocket

hii ya nini, ya wanawake au kwa mahili yeyote au nyumbani for reference. So, mwishowe tutakuwa na kitu kidogo kama hii ya constitution ili kila mtu awe nayo lakini ile kubwa yote itakuwa pia pamoja okay? Okay.

Now imeeleweka Mr. Ludava? Yeah, hiyo four volumes will come, it is being published being done, inachapwa itakuja okay. Haya ile tutazungumzia leo ni hii kitu kiko pia kama South Africa tunayo na mtoto street child au chokora utaenda ukimguza au unfanye nini ukimpiga teke kwa sababu watu wengine wanampiga teke, wanachukua wanasema hii ni Katiba unanidhulumu mimi ni mtoto tena mimi ni mtoto ambaye sina makao unanidhulumu, na akikufanyia hivyo basi, imekuwa hivyo eh. He is protected in the constitution na anaweza kukupeleka kortini kwa vile unemdhulumu, so the constitution protects people in that way and you need to have it, you need to know it, you need to know it very well. Kwa sababu hiyo ndio ita control maisha okay.

Kuna sehemu nyingine iko controlled na maisha yetu yote jumla, iko controlled na Mungu lakini hii ni ya dunia hii. Okay sasa mahali kote Kenya watu wote wanafanya vile tunafanya. We shall finish next week halafu turudi, wacha nimalize hiyo turudi Nairobi.

Kuna National Constitutional Confrence ambayo inakuja mmefanya uchaguzi sivyo, yeah. Hiyo uchaguzi District Coordinator anaweza kueleza lakini National Constitutional Conference ndio inakuja. Hapo tutakuwa na all Members of Parliament 210 elected, tutakuwa na watu watatu kutoka kwa kila district, jana hao watu walikuwa Vihiga watakuja hapa? Yeah, uliwaambia? Wanafaa wajulikane, huyu atawaambia ni wakina nani.

Tutakuwa na representative ya NGOs, representative ya political parties kila watu watakuwa hapo NGO's, people with disabilities watakuwa hapo wanawake watakuwa umo kwa hiyo Confrence. The Confrence venue will be Bomus of Kenya, we had to make a decision you know tuliangalia, tukaangalia Kasarani, tukaangalia nini venues zingine tukasema tutaende Bomus. Itakuwa na watu karibu 700, hao ndio mkutano mkubwa ndio imekuweko hapa Kenya, watu 700 huko a Confrence najua kuna vitu vingine vinaendelea kama delegates ya hii au delegates ya ile, lakini hii nao ni wengi lakini yetu ni Confrence.

Kwa Africa nzima hii ndio Confrence ya constitution kubwa imewekwa. Cameroon walikuwa na 250 delegates, Uganda sijui ilikuwa 400. Wengine walikuwa there is another country which has 350 namna hiyo.. Mozambique pia walikuwa nayo na hivyo, South Africa therefore it was a 500 I think.

Sasa huu mkutano wetu ndio mkubwa sana, hapo role yetu kama Commissioners tutakuwa secretariat hatutakuwa na votes. Hapo tutakuwa tu secretariat, yetu voting ilikuwa kwa kutengeneza draft na hapo ndio majadiliano itakuwa sasa ya nchi na hapo ndio tunajitayarisha sasa, ili wa ofisi wenu wakienda watazungumzia mambo yenu.

So if you have a proposal to make, further proposals you will give them to your representatives. District Coordinator pengine ungetaja tu majina yao halafu wakija baadaye utawainitroduce.

Agnes Ayuma: Commissioner wetu na watu ambao mumejuja kuhudhuria huu mkutano wetu hamjambo.

Audience: Hamjambo.

Agnes Ayuma: Mimi ni Coordinator jina langu ni Agnes Ayuma na last month tulikuwa na uchaguzi kwa wale watu ambao tulikuwa tunataka waende watuwalikishe kwa hii National Constitutional Conference, Nairobi.

Tulikuwa na announcements over the radio na tukawa na, zikawa pia published kwa hizi Daily Newspapers ambazo sisi husoma kila siku, na walikuwa wanataka you pick nomination papers kutoka kwa ofisi ya District Coordinator unajaza, unakuwa na proposer na seconder na subscribers ama supporter, wale watu ambo wana support wewe. Wanasema ya kwamba wewe ni mtu wa character nzuri na unaweza kutuakilisha kwa njia ambayo inafaa. Sasa ilikuwa ni lazima tuwe na moja wa either seconder au proposer awe councilor to the county council.

Tuliweza kupata majina ya karibu watu 15, wanawake wasita na wanaume 9 na tulifanya uchaguzi siku ya Juma nne tarehe 17 mwezi wa September. Tulikuwa pale Vihiga county council na tuliweza kupiga kura na kura zetu ilikuwa kwa njia ya haki na huru, na tulichagua representatives watatu. Mmoja tulipata mwanamke anaitwa Evelia Rebbeca kutoka Hamisi constituency, yeye ndio atawakilisha wanawake kutoka hapa Vihiga district. Wa pili tulipata councilor Calleb Jumba, yeye ndiye Vice chairman Vihiga county council. Na councilor Jumba na councillor Calleb Iganji walipigana vilivyo na councilor Ijumba aliweza kumshinda councilor Iganji kwa kura moja, na akachukua hicho kiti cha Civic leader.

Na tulikuwa na another open seat, ambayo tulipata mshindi kuwa Mr. Charles ohare kutoka Emuhaya constituency. Nadhani mtawaona hapa, watakuja kujijulisha kwenu na hao ndio wale amboa tutatuma kutuakilisha kwa National Constitutional Conference ile ambayo mmesikia itakuwa Bomus of Kenya.

Mnaambiwa ya kwamba makiwa mtakuwa na moani yale mnaona ni lazima isikie Commission na pengine hamna njia ya kufika huko haraka hao watuwakilisha, ukileta hiyo maoni yako tutawapatia na watuwakilisha huko vile wataenda. Asanteni.

Com. Adagala: Asante, nafikiri mimi mwenyewe naweza kusema hiyo ilikuwa fair kwa sababu we are four constituencies in one district na nikaona Emuhaya iko hapo, Hamisi iko hapo na Vihiga constituency iko hapo. Halafu nikaona mimi mwenyewe ninatoka Sabatia pengine ni sawa hao wengine wamepata, sasa tutakuwa huko district nzima yeah. Lakini siku watu walikuwa wanafuata commissioners hata mpaka Mombasa, nataka kukuwa commissioner committee mama Omondi halah! People are voting, unajua the new system will be like that, I mean but people are voting at home why are you in Mombasa? ...oh nataka useme jina langu, tukasema hatuna influence kwa hiyo. Hatukuwa na influence kwa hiyo.

So ni vizuri wamefanya na nimeona ni watu wanatosheka hao ni watu ambao wananguvu kwa sababu kwa National Constitutional Conference itakuwa kama market place of ideas, pia itakuwa kushindana lakini itakuwa kushindana ya vita vya ideas. So I have seen that these are people who can argue and bring up a strong argument.

Ukienda huko na uko maziwa lala au ukienda uko na unatarajia watanipa kitu kidogo kwanza ndio nipige kura utawachwa nyuma. Haya..

Speaker: Are there more comment?

Com. Adagala: Any more comments? Come forward if you have a comment, you just come forward yeah. *(In Kiluhya)*

Heron Odongo: Fine, my names are Haron Odongo Mkangula and I come from Kigama sub location and mine is a question also a kind of observation, that already we are supporting the Constitutional Review Commission going on in Kenya and this is historical in our country. And that we are sometime very much hurt when we hear a create space few politicians say that this constitution is better suited for foreigners, but I have been going through and I found out, it is a very good constitution for our ages to come. It will benefit us and it will also benefit those who are coming a head of us. So my question is what is the role of the Constitution Review Commission? Are they able, do they have the ability to stop these politicians from making it naïve or trying to pre-desitinate it kind of something of that kind, yeah. That is my question.

Ludaga: Sorry I thought we were making a comment just on elections. I think on the on set mimi naona hawa watu tumechagua wametulet down, maanake kama huu mkutano ilitakikana kuanza saa nne na sasa ni saa tano na dakika kumi na tano. Sisi tayari tunapeana views ambazo hawa watu walichaguliwa wanatakikana wawe wakichukua notes na kuakilisha kwa ile confrence, na saa hii hawajakuja, tunaambiwa watajitokeza saa ile pengine sisi tushaenda. Mimi sioni kama hii ni vuzuri. That is one.

Two, nafikiri nationally pengine constitutional Review Commission, ingekuwa imefanya mipango ambao wale wakilishi tuliochagua wangekutana na watu wa hiyo district ili wawe kama wanabeba maoni yao kabisa wakienda huko ili tujue kwamba wakati wakienda, wameenda kutuakilisha kikamilifu. Asante.

Com. Adagala: Hii ndio forum wanatakikana wawe walikuwa Vihiga wakija utatoa hiyo comment eh. La pili, tulikuja kuchukua views kutoka kwenu, zile views tuliambiwa kwa sheria collect and collate. To collect and then put together na tuna database ina hiyo computer ambayo ina hizo views zote. Sasa, maoni yenu yote iko kwa hiyo computer lakini mkikubali nyinyi ni foreigners, that is what they are saying, you people are foreigners. So who are Kenyans? You need to answer because we got these views from you, kuna format ambayo constitution zote duniani zinafuata eh. Standard format, standard ways of writing them. So we have it that way, so if there is foreign views then you are foreigners. Nyinyi ni wageni si Wakenya?

Audience: Si wageni.

Com. Adagala: Views ya Wakenya ziko hapa. Mnajua kuna kitu kinaendelea Kenya inabadilika mtu mwingine alisema how can we silent the politicians, we shall not silent the politicians, their right is here, freedom of expression, uhuru wa kusungumza, uhuru wa kusikika uko hapa, okay. Lakini wamezoea wao ndio wanazungumza na watu wengine hawezungumzi hiyo ni mtindo wa 20th century. Tunaenda kwa 21st century, mkitaka twende 21st century, tuende, ukitaka ubaki 20th century eh, 1999, 1950, 1963, 1978, 1988, hakuna mtu atakukataza. Lakini tunaona tuna views ya majority hapa, hiyo ndio tulikuwa tunasikizana kwa hiyo mkutano Mombasa.

What did the majority of the people say, halafu extreme view ilikuwa hii na maoni nyingine ilikuwa hii na ingine extreme ilikuwa ile. Na majority walisema hivi, mimi ni mtafiti I am reseacher nimefanya researche more that 20 years, that is how you collate views. Views ile ilikuwa on the Judiciary ni 1800 pages, 90%, 99% even if I have one to say of those views are all negative ya Mahakama, vile wananchi wako treated mahakamani ni negative. Sasa tusema aje tubadilishe tuseme hao watu wakubwa watajiri sana hatuwezi, tungefanya hivyo mngeskataa mngesema hatukusema hivyo okay.

So we can not stop the politicians, the politicians have a right, you have a right okay, isipokuwa magazeti yetu inareport mambo ya watu wakubwa, lakini wangukuwa fair wangukuwa hapa wareport mambo yenu pia Yeah. So those views we can only take them and put them on record we cannot put much than that okay.

Katiba tunatengeneza Kenya mpya ukitaka kubaki kwa ile Kenya ya zamani ni sawa tu, your right. Politicians have a right of associantion eh, you have right of association. You can associate with your views and associate with them, it's okay. You can also associate with whoever you want to associate. Kenya huru inakuja na iko njiani, na mzoe kubishana sio kupigana lakini kubishana kwa maoni na kujadiliana hiyo ndio democracia. Unasikiliza huyu lakini ni pia ni democracia mila yetu (*In Kiluhya*) halafu unakwisha hapo eh, (*In Kiluhya*). Hiyo ndio haki, haki ya tovu, kuna haki ile ya tovu (*In Kiluhya*) hiyo mtu hawezi kukunyanganya okay. Haya basi tuendelee na hii basi.

Speaker:(?).

Com. Adagala: Ukiwa na swali Mzee unakuja mbele, sitaki kelele kutoka huko.

Speaker:(?).

Com. Adagala: Utakuja, utatembea na miguu yako uje hapa na ninaambia kila mtu.

Lazarus Samba: Jina langu ni Lazarus Samba, mimi natoka hapa Chavakali. Swali ile ningependa kuuliza wananchi au kuuliza commissioner ni hili hapana uliza commissioner.

Interjection Com. Adagala: Angalia huko, angalia(?)

Lazarus Samba: Kwa nini au tungekuwa na kufungu ndani ya Katiba yetu hii, ilikuwaaje mtu kama Rais wetu alikataa kutoa maoni yake kwa Katiba yetu. Na tena close up this space yeye amekuwa msitari wa mbele kulaumu Katiba yetu. Je mnaweza zozanaje na mtu ambaye hamkulima naye shamba? Mimi naonelea hivi, mtu yeyote ambaye hakutoa maoni yake hana haki ya kutoa makosa Katiba yetu. Mmoja akiwa Rais, anakosa sana.

Tukiendelea mbele hawa Majudge wanataka kushtaki Katiba yetu, mbona tunaona hii Katiba ya zamani ni mbaya sana sana, hata imefanya nchi yetu imefilisika mbona hawakuteta. Ni Katiba mbaya, sasa yetu ndio wanaona ni mbaya, hatutaki maneno yao, wao ndio wanaona tunataka kujua ufisadi wao, ufisadi inanzia mahakamani. Sasa tunataka kuzuia huo ufisadi isianguksha nchi yetu na wanaanza sasa kupeleka Katiba yetu kortini vipi!

Sasa mimi swali langu ilikuwa tukienda kongomano huko mnataka kwenda huko tukatae wile watu hawakutoa maoni mmoja akiwa Rais, asizungumze, asidhubutu kulaumu Katiba yetu. Sasa hii ya zamani yeye hakuenda Lancaster house.

Audience: Alienda.

Lazarus Samba: Alienda na kama alienda? Na kama alienda mimi sikumsikia akiteta, nilisikia some, nilisikia akina Tom Mboya, akina Muliro akina nani. Lakini Rais wetu sikusikia maoni yake. Ya Shikuku nilisikia, bas hivyo hivyo ni ana complain kwa kuwa wamemnyanganya Rais madaraka. Wasi ni hii, Katiba ilioko sasa, wananchi walifanya vizuri sana wakaweka Rais juu ya sheria ambayo vile vile ilikuwa ni kosa. Sheria ya kuweka mtu juu ya sheria ni, juu ya sheria ni Mungu peke yake.

Hata Katiba ya zamani ilikuwa na makosa, mtu kuwa juu ya sheria ni Mungu peke yake. Lakini mbona wananchi hawakuona hiyo Katiba ni mbovu. Sasa hii yetu ndio wanaona ni mbovu, inaheshimu Mungu wao wanasema hiyo ni mbaya. Nini hii?

Murmering from the audience

Basi, machache ni hayo lakini wakati nilisikia wanashtaki Katiba hata ugali mimi sishibi. (*Laughter from the audience*). Imefanana ni mimi ndio wanatengeneza hiyo, si hiyo hiyo mbaya kabisa.

Com. Adagala: Kuna haki ya kuzungumza lakini muda ndio imekwisha.

Lazarus Samba:(Inaudible).

Com. Adagala: Lakini tumechukua hiyo ni proposal yako, tumeichukua umeiandika, proposals yake? Asante Mzee, Samba asante. Ah okay, nafikiri hakuna mambo, ya maana ya ku nini hapo kwa sababu Mzee ni Mzee ambaye ana historia mnaona kwa nywele yake sivyo?

Okay tuendeleo, tutaenda haraka haraka kidogo eh. Haya angalieni kwa table of contents peke yake. Does this thing have table of content does it say so. Okay kuna karatasi ya kwanza hiyo table of contents eh. Tutasoma kidarasa. You don't have a driver.....(?). Okay tunaita driver alete gari tuchukua more constitution reports from it. Hapo, kuna kitu kinaanza table of contents eh, mnaona kuna kitu hapo preamble. Preamble ni utangulizi, mtaona kwa Kiswahili ni utangulizi, hiyo sehemu haiko kwa Katiba ya sasa, haiko ndani ndio hiyo tumeongeza kwa sababu wananchi walisema lazima tuwe na utangulizi na pia tuwe na mambo ambayo inatuongoza kwa Kenya hiyo iko hapo.

Chapter ya kwanza ni hiyo ambayo inaleta ile ukubwa ukuu, ile ni ya ukuu sovereignty. Ukuu Mzee amesema juu ya Katiba ni Mungu lakini hapa tunasema wakuu wa Katiba ni wananchi, hiyo iko hapo na ukuu wenyewe halafu kuna sehemu hapo tutazungumzia hata tutazumzia constitution ni nini hapo.

Chapter ya pili ni the republic, okay. Kwa Katiba ya sasa hiyo vitu tumezungumzia preamble na hiyo chapter ya kwanza haiko. Inaanza tu Kenya is a sovereign republic, kwa sababu Muingereza alitaka kutupea nchi yetu, sasa yeye alianza tu hivyo. Kazi yake ilikuwa kupeana nchi Kenya is a sovereign republic. Lakini hapo tumefafanua zaidi na tunazungumzia republic hii ni nini? Inaendelea vipi? Ina nani ndani? Na ramani yake ni nini? Where is the map of it, eh (*In Kiluhya*) okay, haya.

Chapter three ni national goals and principles, hatuna kwa Katiba hatuna kitu ambacho kinatuongoza sasa tumepata vile mlikuwa mnasema. Sisi tukiwa watu wa Kenya, nia yetu ni nini? Lengo letu ni nini? Ni nini tunaheshimu kwa maisha yetu? Hayo yako hapo yote na hiyo pia kuongozwa na Principal. Hiyo ni kitu muhimu unajua siku hizi ukiambia mtu lazima ufanye maendeleo hakuna lazima, hao watu wanafanya kwa hiari, wanafanya vitu vingine kupata kura, au kwa sababu wanapenda maendeleo kuna watu kama hao, wanafanya tu kwa sababu wanapenda maendeleo lakini hapa tukifika hapo lazima iwe na hiyo goal, tutazungumzia hizo.

